JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

EAST AFRICAN COMMUNITY
LAKE VICTORIA BASIN COMMISION



# SIKU YA ZIWA VICTORIA 2026

“Maji Yetu, Mustakabali Wetu: Tuungane kwa Uendelevu wa Bonde la Ziwa Victoria.”




“ZIWA LETU
FAHARI YETU”

# UTANGULIZI

Karibu katika jarida hili linalohusu uzinduzi wa Siku ya Ziwa Victoria iliyofanyika Jijini Mwanza na Kuongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Maadhimisho ya Kwanza ya Siku ya Ziwa Victoria yametokana na Azimio la Mkutano wa 23 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria uliofanyika tarehe 16 Mei 2025 jijini Kisumu nchini Kenya.

Mkutano huo uliipitisha tarehe 21 ya mwezi Mei kila mwaka kuwa Siku ya Ziwa Victoria na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliombwa na kuridhia kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya kwanza.

Maadhimisho haya yalifanyika kwa siku Nne kuanzia tarehe 18 hadi 21 Mei 2026. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na; maonesho ya wanyama hai aine Nne ambao ni Fisi, Simba, Ngamia na Farasi pamoja na vikundi vya utamaduni na burudani.

Mei 18, 2026; kulifanyika shughuli za uhifadhi wa mazingira ya Ziwa Victoria ambapo zaidi ya miti 5,000 rafiki wa maji ilipandwa kwenye Chanzo cha Maji Butimba. Kazi hii iliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda huku Wizara ya Maji ikiwakilishwa na Naibu Katibu Mkuu Bi. Rose Ambrose.

Kazi ya Pili ilikuwa ufunguzi wa maonesho ya shughuli mbalimbali zinazohusiana na maji, ubunifu na tamasha la utamaduni katika viwanja vya Nane Nane. Wadau zaidi ya 50 wanaojumuisha Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Washiriki kutoka Jamhuri ya Kenya, Wajasiliamali, Jumuiya za Watumia Maji, Taasisi za Madini, Vikundi vya Jamii, Taasisi za Watafiti, na Viwanda Vidogo walishiriki.

Pia kulikuwa na Warsha kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Maji kwa ajili ya uvuvi endelevu iliyoratibiwa na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani. Zaidi ya watu 50 kutoka Taasisi na Nchi mbalimbali walishiriki.

Mei 19, 2026 kulifanyika Mkutano wa Jukwaa la Wadau wa Bonde la Ziwa Victoria. Zaidi ya wadau 200 kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Kimataifa walishiriki.

Mei 20, 2026 kulifanyika mkutano wa Wadau wa Maendeleo wa Bonde la Ziwa Victoria. Mkutano huo ulihudhuriwa na Viongozi wa Serikali za Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Wadau wa Maendeleo. Wadau hao ni pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNDP na FAO, Benki ya Dunia, EADB, EU, Ubalozi wa Marekani, GIZ, na WWF. Mkutano ulibainisha fursa za uwekezaji kwenye Bonde la Ziwa Victoria.

Pia kulifanyika mchapalo kwa ajili ya kuwakaribisha Wageni kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wadau wa Maendeleo na Jumuiya ya Kimataifa. Aidha tukio hili liliambatana na utoaji wa zawadi na vyeti katika makundi mbalimbali ikiwemo Vijana wanaofanya Utafiti katika Bonde la Ziwa Victoria kutoka Vyuo Vikuu vya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Wanawake Vinara wa Mabadiliko ya Shughuli za Uhifadhi wa Mazingira ya Bonde la Ziwa Victoria; Taasisi zenye mifumo bora ya Uhifadhi majitaka; Wabunifu wa Mfumo wa Akiliunde wa Kufuatilia Ubora wa Maji katika Vizimba vya Samaki; na Waoneshaji katika mabanda ya maonesho.

Tarehe 21 Mei 2026 ilikuwa ni kilele cha Siku ya Ziwa Victoria. Siku hiyo kulifanyika Uzinduzi rasmi wa Siku ya Ziwa Victoria na ukamilishaji wa Maadhimisho ya Kwanza ya Siku ya Ziwa Victoria ambayo yaliongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.



# DKT. MWIGULU AWASILI MWANZA KUONGOZA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA ZIWA VICTORIA











# Hotuba ya Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb) Siku ya Ziwa Victoria



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba alizindua Siku ya Ziwa Victoria huku akiwashukuru wadau wote waliowezesha tukio hilo muhimu. Alisema maji ni kila kitu katika maendeleo na uhai wa binadamu kwani hayana mbadala. Alishukuru jitihada ambazo zimekuwa zikifanyika kuhakikisha ziwa hilo linalindwa, linatunzwa na kuendelezwa kwa ajili ya vizazi vya sasa na baadaye. Alitoa maagizizo mbalimbali huku akisisitiza;

•Kazi ya utunzaji na uendelezaji wa Ziwa Victoria iwe endelezu na ishirikishe jamii nzima inayozunguka ziwa kwa kuiishi Kaulimbiu ya Siku ya Ziwa Victoria ambayo ni **"Maji Yetu, Mustakabali Wetu: Tuungane kwa Uendelevu wa Bonde la Ziwa Victoria."**

•Mikakati ya utunzaji wa ziwa ihusishe kuwaandaa vijana wadogo kufahamu umuhimu wa ziwa hilo kwa kuanzisha vilabu na mashindano shuleni ambayo yatakuwa yakihamasisha utunzaji wa Ziwa Victoria

•Vituo vya kuratibu utafutaji na uokoaji ndani ya ziwa Victoria viendelezwe na kupewa msisitizo katika maeneo yote yanayozunguka ziwa Victoria

•Taasisi za utafiti zifanye utafiti wa kina kubaini na kupata suluhisho la kudumu la magugu maji ndani ya ziwa Victoria.





# Hotuba ya Waziri wa Maji Mheshimiwa. Jumaa Aweso Siku ya Ziwa Victoria



Waziri Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) alisisitiza kuwa Ziwa Victoria ni urithi wa pamoja unaounganisha mataifa ya Afrika Mashariki kupitia uchumi, mazingira, biashara, utamaduni na maisha ya mamilioni ya wananchi wanaolitegemea kila siku. Ziwa Victoria si chanzo cha uchumi pekee bali pia ni suala muhimu la usalama wa nchi na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisisitiza kuwa Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuwekeza katika miradi ya maji ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora. Kauli yake, "No Blue, No Green; No Green, No Nation," inaonesha umuhimu wa kulinda rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu.

Katika Mkoa wa Mwanza, Serikali inatekeleza miradi ya Ukiliguru, Sumve na Koromije yenye thamani ya shilingi bilioni 32.76, itakayowanufaisha wananchi zaidi ya 162,000.



**Mradi wa Maji Butimba**

Aidha, awamu ya kwanza ya Mradi wa Butimba imekamilika kwa kujenga chanzo na kituo cha kutibu maji chenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 48 kwa siku. Ukarabati na upanuzi wa kituo cha Capripoint unaendelea na utaongeza uzalishaji wa maji hadi kufikia lita milioni 144 kwa siku. Sambamba na hilo, ujenzi wa matenki matano ya kuhifadhi maji pamoja na miradi ya kuboresha huduma katika maeneo ya Kisesa, Buswelu, Luchelele, Buhongwa, Kishiri na Usagara utaimarisha upatikanaji wa maji kwa mamia ya maelfu ya wananchi.




Katika Mkoa wa Simiyu, Serikali inatekeleza Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 440 utakaowanufaisha wakazi wa Wilaya za Bariadi, Busega na Itilima pamoja na vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu la maji.

Vilevile, kupitia Mradi wa Miji 28 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.58, miradi ya maji inaendelea kutekelezwa katika miji mbalimbali ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Mugumu, Chato, Geita, Tarime na Rorya. Mkoa wa Mara pia unaendelea kunufaika kupitia miradi ya Butakale, Kisangwa, Wariku, Kibara, Nyamswa na mradi wa maji wa vijiji 24 vya Jimbo la Mwibara. Aidha, miradi mingine inaendelea katika Wilaya ya Nzega na maeneo ya Nkome, Katoma, Nyamboge, Nzera na Lwezera, ambapo maelfu ya wananchi watanufaika na huduma ya maji safi na salama.

Alihitimisha kwa kusisitiza Mshikamano wa wananchi wote wanaounda Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ili kuhakikisha ziwa Victoria linalindwa na kuendelezwa.

# Salamu za Dkt. Nancy Koech, Naibu Mkurugenzi Mkuu, Wizara ya Maji Kenya katika Jukwaa la Wadau wa Bonde la Ziwa Victoria



Mkutano wa Jukwaa la Wadau ulifanyika Mei 19, 2026 jijini Mwanza. Katika mkutano huo Dkt. Koech alisema Ziwa Victoria ni rasilimali muhimu inayochangia maendeleo ya Afrika Mashariki kupitia uvuvi, biashara, kilimo, usafirishaji, utalii na urithi wa kitamaduni. Hata hivyo, ziwa linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira, kupungua kwa samaki, kuenea kwa viumbe vamizi na ongezeko la watu. Changamoto hizi zinahitaji ushirikiano wa kikanda na ushiriki wa wadau wote.



Alisema serikali ya Kenya inaamini kuwa uhifadhi na matumizi endelevu ya Ziwa Victoria yanawezekana kupitia ushirikiano wa serikali, jamii, sekta binafsi, taasisi za utafiti, asasi za kiraia na washirika wa maendeleo. Majukwaa kama haya yanatoa fursa ya kubadilishana uzoefu na kupanga hatua za pamoja za kulinda ziwa na kuboresha maisha ya wananchi.



Alisisitiza maadhimisho ya kwanza ya Ziwa Victoria yasaidie kuimarisha dhamira ya kuendeleza uchumi wa buluu, kulinda mazingira na kuimarisha ushirikiano wa kikanda. Kwa upande wa Kenya, Serikali imejipanga kupanda zaidi ya miti milioni moja kila mwaka katika maeneo ya vyanzo vya maji vinavyoingia Ziwa Victoria na inaendelea kupitia sera na kanuni za usimamizi wa rasilimali za ziwa ili kuimarisha matumizi endelevu.

Alihitimisha kwa kuwatakia washiriki wote mijadala yenye tija na ushirikiano wenye manufaa kwa maendeleo na ustawi wa Afrika Mashariki.

# Hotuba ya Dkt. Alfred Okot OKid, Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Mazingira Uganda



Ninapenda kuishukuru Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuandaa na kuwa wenyeji wa kongamano hili muhimu la wadau. Pia naleta salamu za dhati kutoka Serikali na wananchi wa Uganda, hususan kutoka Wizara ya Maji na Mazingira.

Ziwa Victoria ni moja ya rasilimali muhimu zaidi katika Afrika Mashariki. Mbali na kuwa ziwa kubwa zaidi la maji safi barani Afrika, lina mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa mamilioni ya wananchi. Bonde hili linahudumia watu kati ya watu milioni 45 hadi 50 kupitia huduma za maji, uvuvi, usafiri, biashara, kilimo, utalii, uzalishaji wa umeme wa maji na uhifadhi wa bioanuwai. Kwa hiyo, mustakabali wa wananchi wetu umefungamana kwa kiasi kikubwa na afya na uendelevu wa ziwa hili.

Kaulimbiu ya maadhimisho haya ya kwanza ya Siku ya Ziwa Victoria, “Maji Yetu, Mustakabali Wetu: Tuungane kwa Uendelevu wa Bonde la Ziwa Victoria,” inatukumbusha umuhimu wa kufanya kazi kwa pamoja katika kulinda na kusimamia rasilimali hii ya pamoja. Hakuna nchi moja inayoweza kukabiliana peke yake na changamoto zinazolikabili bonde hili; ushirikiano wa kikanda ni jambo la msingi.




Pamoja na umuhimu wake mkubwa, Bonde la Ziwa Victoria linakabiliwa na changamoto nyingi zinazoongezeka kutokana na ukuaji wa haraka wa idadi ya watu, maendeleo ya miji na viwanda, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa maeneo ya vyanzo vya maji, kupungua kwa ardhi oevu na athari za mabadiliko ya tabianchi. Changamoto hizi zinaongeza shinikizo kwa rasilimali za maji na kuhatarisha ustawi wa mifumo ya ikolojia inayotegemewa na wananchi wetu. Mojawapo ya changamoto kubwa ni kushuka kwa ubora wa maji kutokana na kutiririshwa kwa maji taka kwenye mazingira bila kutibiwa ipasavyo. Hali hii inachangia kuongezeka kwa uchafuzi wa maji, kuathiri viumbe wa majini na kuhatarisha afya za wananchi wanaotegemea ziwa kwa matumizi mbalimbali. Aidha, athari za mabadiliko ya tabianchi zimeendelea kujitokeza kwa namna mbalimbali, ikiwemo mafuriko makubwa yaliyoshuhudiwa katika miaka ya hivi karibuni ambayo yalisababisha uharibifu wa miundombinu na kuathiri maisha ya maelfu ya wananchi katika nchi za Uganda, Kenya na Tanzania. Usalama wa usafiri majini pia unapaswa kupewa kipaumbele.

i muhimu kwa ustawi wa wananchi wetu na maendeleo ya ukanda wa Afrika Mashariki kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Ziwa Victoria ni njia muhimu ya usafiri, biashara na uvuvi, lakini bado ajali za majini zinaendelea kugharimu maisha ya watu wengi. Hivyo, kuna umuhimu wa kuimarisha mifumo ya tahadhari za mapema, utoaji wa taarifa za hali ya hewa na hatua nyingine za kuimarisha usalama wa watumiaji wa ziwa. Kwa upande wa Uganda, tunaendelea kutoa kipaumbele katika usimamizi endelevu wa Bonde la Ziwa Victoria kwa kutambua mchango wake katika usalama wa maji, chakula, nishati na mazingira.

Tutaendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, washirika wa maendeleo na wadau wengine katika kutafuta suluhisho la pamoja kwa changamoto hizi. Ninatoa wito kwa wadau wote kuendelea kuwekeza katika hatua za vitendo zitakazochangia ulinzi na maendeleo endelevu ya bonde hili. Kwa kufanya kazi kwa pamoja, tunaweza kuhakikisha kuwa Ziwa Victoria linaendelea kuwa rasilimal



## Hotuba ya Dkt. Masinde Bwire, Katibu Mtendaji, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, katika Maadhimisho ya Siku ya Ziwa Victoria, Mwanza



Dkt. Masinde alisema. Ziwa Victoria ni chanzo cha maisha kwa zaidi ya watu milioni 45 katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na linachangia maendeleo kupitia sekta za uvuvi, kilimo, usafirishaji, utalii, uzalishaji wa nishati, biashara, bioanuwai na urithi wa kitamaduni.

Pamoja na umuhimu wake, Ziwa Victoria linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uchafuzi wa mazingira, taka za viwandani na majumbani, plastiki, kilimo kisicho endelevu, ukataji miti, uharibifu wa ardhi oevu, viumbe vamizi na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, ongezeko la watu na ukuaji wa miji vinaendelea kuongeza shinikizo kwenye mfumo wa ikolojia wa ziwa. Ripoti ya Hali ya Bonde na Mkakati wa Usimamizi Jumuishi wa Rasilimali za Maji imeainisha changamoto hizi pamoja na fursa zilizopo za kuboresha usimamizi wa bonde.

Katika sekta ya uvuvi, uvuvi haramu na wa kupita kiasi unaendelea kuhatarisha rasilimali za samaki na maisha ya wananchi. Hivyo, kuna umuhimu wa kuoanisha kanuni za uvuvi kati ya nchi wanachama, kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na utekelezaji, kuendeleza usimamizi shirikishi wa uvuvi na kuweka mazingira ya vyanzo mbadala vya kipato kwa jamii zinazotegemea ziwa.



Vilevile, alisisitiza uwekezaji katika mipango endelevu ya miji, usimamizi wa maji taka, urejeshaji wa mifumo ya ikolojia na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Katika sekta ya usafiri wa majini, changamoto za usalama, ajali na miundombinu zinahitaji kushughulikiwa.

Uanzishwaji wa Kituo cha Kisasa cha Uratibu wa Uokoaji Majini Marine Rescue Coordination Center-**MRCC** Ilemela, Mwanza ni hatua muhimu ya kuimarisha usalama wa majini na ushirikiano wa kikanda.

Uhifadhi wa Ziwa Victoria ni wajibu wa pamoja unaohitaji ushirikiano wa serikali, jamii, sekta binafsi, taasisi za utafiti, mashirika ya kiraia na washirika wa maendeleo. Tunapaswa kuimarisha matumizi ya tafiti, ubunifu, ushirikiano wa data na uratibu wa sera ili kuhakikisha maamuzi sahihi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Tukilinda Ziwa Victoria, tunalinda maisha ya wananchi wetu, uchumi wetu, mazingira yetu na mustakabali wa Afrika Mashariki.

# HABARI PICHA





Waziri mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba akiwasili katika viwanja vya Nanenane Nyamhongolo jijini Mwanza kwa ajili ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ziwa Victoria, ambapo alipokelewa na mwenyeji wake, Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali na Sekta ya Maji.

Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba akitembelea mabanda mbalimbali ya maonyesho katika Maadhimisho ya Siku ya Ziwa Victoria yanayofanyika katika viwanja vya Nanenane Nyamhongolo jijini Mwanza, akiwa ameambatana na mwenyeji wake Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb). Waziri Mkuu amepokea maelezo kutoka kwa wadau mbalimbali wanaoshiriki maonyesho hayo kuhusu shughuli na jitihada za uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji.





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akisalimiana na viongozi mbalimbali mara baada ya kuwasili katika viwanja vya Nanenane Nyamhongolo jijini Mwanza, katika Maadhimisho ya Siku ya Ziwa Victoria yenye kaulimbiu: "Maji Yetu, Mustakabali Wetu: Tuungane kwa Uendelevu wa Bonde la Ziwa Victoria."









Katibu Mkuu Wizara ya Maji Engineer Mwajuma Waziri akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Sekta ya Maji wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ziwa Victoria yanayofanyika katika viwanja vya Nanenane Nyamhongolo jijini Mwanza, yakiongozwa na kaulimbiu isemayo: "Maji Yetu, Mustakabali Wetu: Tuungane kwa Uendelevu wa Bonde la Ziwa Victoria."



Naibu Katibu Mkuu WIzara ya Maji Bi, Rose Ambrose akipokea zawadi kutoka kwa Katibu Mtendaji Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria Dkt. Masinde Bwire




Picha mbalimbali zikionesha makundi tofauti ya wageni waliohudhuria Maadhimisho ya Siku ya Ziwa Victoria yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane Nyamhongolo jijini Mwanza, yakiwajumuisha viongozi wa Serikali, viongozi wa dini pamoja na wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji kutoka ndani na nje ya nchi.

Washiriki hao walijitokeza kushuhudia maadhimisho hayo ya kihistoria yaliyolenga kuhamasisha uhifadhi wa Ziwa Victoria, matumizi endelevu ya rasilimali za maji pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda kwa maendeleo ya Uchumi wa Bluu katika Afrika Mashariki.




Wadau wa sekta ya maji wakishiriki kupanda miti katika chanzo cha maji cha mradi wa maji Butimba Mei 18, 2026,

Miti zaidi ya 5,000 rafiki wa Maji Ilipandwa.




Mkutano wa Wadau wa Maendeleo wa Bonde la Ziwa Victoria. Mkutano huu ulihudhuriwa na Viongozi wa Serikali za Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Wadau wa Maendeleo. Ambao ni pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNDP na FAO, Benki ya Dunia, EADB, EU, Ubalozi wa Marekani, GIZ, na WWF.




Sanaa na Utamaduni ni sehemu ya burudani zilizopamba maadhimisho ya siku ya ziwa Victoria




Ripoti ya hali ya Bonde la Ziwa Victoria kwa Mwaka 2025 ilizinduliwa katika siku ya ziwa Victoria

# YALIOJIRI
## SIKU YA ZIWA VICTORIA



















# Serikali Yataka Ulinzi Na Uhifadhi Wa Ziwa Victoria

**Waziri Mkuu Mhe. Nchemba**

*Serikali imesisitiza umuhimu wa ulinzi wa ziwa Victoria kwa maendeleo ya wananchi.*

Dkt. Mwigulu Nchemba amesema hayo katika maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Ziwa Victoria yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane Nyamhongolo jijini Mwanza,.

Dkt. Mwigulu, mgeni rasmi wa siku hiyo, amesema ziwa Victoria ni rasilimali ya pamoja inayopaswa kulindwa na kuhifadhiwa kwa ushirikiano wa kikanda kutokana na mchango wake mkubwa katika uchumi, biashara, mazingira, usalama na maisha ya wananchi.

***"Ziwa Victoria si mali ya nchi moja. Ni rasilimali inayotuunganisha kama jumuiya na tunapaswa kushirikiana katika kulinda mazingira, usalama na uchumi unaotegemea ziwa hili,"*** *Dkt. Nchemba amesema.*

Amesema maadhimisho hayo yanapaswa kuwa sehemu ya kuhamasisha usimamizi endelevu wa rasilimali za maji, kuimarisha mshikamano wa kikanda pamoja na kuongeza uwajibikaji wa pamoja katika kulinda mazingira ya ziwa Victoria kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Amesisitiza umuhimu wa kuimarishwa kwa mifumo ya usalama na uokoaji majini pamoja na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika kufuatilia shughuli za uvuvi, ubora wa maji na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ametoa wito kwa taasisi za utafiti kuendelea kufanya tafiti zitakazosaidia kupata suluhisho la changamoto zinazoathiri mazingira ya ziwa Victoria ikiwemo ongezeko la magugu maji na uharibifu wa vyanzo vya maji.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji katika Kanda ya ziwa pamoja na kuimarisha juhudi za kulinda na kuhifadhi ziwa Victoria ambalo ni nguzo muhimu ya uchumi, usalama na maendeleo ya wananchi.

Sanjari na hayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri amesema Tanzania imekuwa mwenyeji wa kwanza wa maadhimisho hayo kufuatia maamuzi ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Amesema maadhimisho hayo yamehusisha shughuli mbalimbali ikiwemo kuotesha miti, maonesho ya wadau wa Sekta ya Maji pamoja na mijadala kuhusu uhifadhi wa Ziwa Victoria.

Kaulimbiu ya maadhimisho ni : *"Maji Yetu, Mustakabali Wetu:* Tuungane kwa Uendelevu wa Bonde la Ziwa Victoria" na yamehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, wananchi, wadau wa Sekta ya Maji pamoja na wageni kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.



# Miti Yaoteshwa Butimba Siku Ya Ziwa Victoria

**Butimba**, *Mwanza*

Wananchi katika Mkoa wa Mwanza wameshiriki kampeni ya kutunza vyanzo vya maji katika ziwa Victoria kwa kuanza kuotesha miti elfu mbili katika chanzo cha maji cha Butimba.

Mkuu wa mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Said Mtanda ameongoza zoezi hilo ambapo miti rafiki wa maji imeoteshwa kuashiria uzinduzi wa kampeni ya kuotesha miti kuelekea siku ya ziwa Victoria ambayo inaadhimishwa kwa mara ya kwanza Jijini Mwanza.

Amesema Ziwa Victoria linanufaisha watu zaidi ya milioni 45 wa Afrika Mashariki hivyo ni muhimu kuhakikisha linahifadhiwa na kuendelezwa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Amesema kupanda miti ni kumbukumbu kubwa inayodumu hata aliyepanda anapokuwa hayupo.

Amewataka wananchi wote kuhakikisha wanaendelea kuotesha miti katika vyanzo vyote vya maji, makazi na maeneo mbalimbali kwasababu miti ni mazingira, mazingira salama ni maisha salama.

Amesisitiza kuwa mstakabali wa jiji la Mwanza ni uwepo wa ziwa Victoria kwa sababu miradi mikubwa ya kimkakati ya maji ukiwemo mradi wa maji wa Butimba chanzo chake ni ziwa Victoria.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Bi. Rose Ambrose amesema Wizara ya Maji imejipanga kuhakikisha wananchi wa Mwanza wananufaika na rasilimali ya maji kwa kuhakikisha ulinzi na uendelezaji wa ziwa Victoria unapewa kipaumbele.

Zoezi la kuotesha miti limewashirikisha viongozi mbalimbali akiwamo Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Rose Ambrose ambaye amesisitiza umuhimu wa kuotesha miti katika vyanzo vya maji vyote nchini. Amesema Wizara ya Maji kupitia Bonde la Ziwa Victoria inakusudia kuotesha miti 10,000. Ambapo miti 6500 imeshaoteshwa. Aidha pamoja na miti 2000 iliyooteshwa, Wizara ya Maji inakusudia kuotesha miti 5000 katika maadhimisho ya siku ya Ziwa Victoria ambayo ni Mei 21.



Amesema chanzo cha maji cha Butimba ni muhimu kwa maisha ya wakazi wa Mwanza kwasababu chanzo hicho kinazalisha lita za maji kwa siku milioni 48 na kunufaisha zaidi ya wananchi 450,000. Lengo ni kukiendeleza ili kifikie uzalishaji wa maji lita milioni 96 ambazo zitakuwa zikinufaisha wakazi laki nane.

Naye Katibu Mtendaji Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria Dkt. Masinde Bwire amesema zoezi la kuotesha miti katika kutunza ziwa Victoria linafanyika kwa nchi zinazounda kamisheni hiyo zikiwemo Kenya, Uganda Burundi na Rwanda

Amesisitiza ushirikiano kwa kila mmoja ili kuhakikisha ziwa hilo linadumu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.







# Ushirikiano Wahitajika Kutunza Ziwa Victoria

**Saidi Mtanda,**
*Mkuu wa Mkoa wa Mwanza*

*Ushirikiano na ushirikishwaji wa jamii unahitajika katika kutunza ziwa Victoria*

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Said Mtanda amewataka wananchi wa eneo la kamisheni ya Bonde la ziwa Victoria kushirikiana katika utunzaji wa rasilimali maji ya ziwa hilo.

Amesema hayo akifungua maonesho kuelekea siku ya Ziwa Victoria ambayo itafanyika Mei 21.

Maonesho yanafanyika katika eneo la Nyamongoro viwanja vya Nanenane jijini Mwanza ambapo mgeni rasmi katika siku ya ziwa Victoria anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba.

Mkuu wa Mkoa Bw. Mtanda amesema Ziwa Victoria lina umuhimu mkubwa kwa wananchi wote za nchi za Afrika Mashariki hivyo ushirikiano wa dhati unahitajika kuwezesha rasilimali hiyo kuendelezwa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Amesisitiza kuwa mstakabali wa jiji la Mwanza ni uwepo wa Ziwa Victoria kwa sababu miradi mikubwa ya kimkakati ya maji ukiwemo mradi wa maji wa Butimba chanzo chake ni ziwa Victoria.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Bi. Rose Ambrose amesema Wizara ya Maji imejipanga kuhakikisha wananchi wa Mwanza wananufaika na rasilimali ya maji kwa kuhakikisha ulinzi na uendelezaji wa ziwa Victoria unapewa kipaumbele.



Siku ya Ziwa Victoria inatarajiwa kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa nje na ndani ya nchi wakiwemo nchi zinazounda Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, nchi za Tanzania, Kenya Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.



# Wadau Wakaribishwa Kuwekeza Uhifadhi Ziwa Victoria

**Bi. Rose Ambrose** , *Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji*

*Wadau wa Sekta ya Maji wamekaribishwa kuwekeza katika uhifadhi wa ziwa Victoria.*

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Bi. Rose Ambrose amewaalika wadau wa maendeleo kuwekeza katika uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za maji za Ziwa Victoria.

Amesema hayo akifungua warsha ya wadau wa Bonde la Ziwa Victoria katika Maadhimisho ya kwanza ya Ziwa Victoria jijini Mwanza.

Amesema kazi ya uhifadhi na uendelezaji wa ziwa Victoria inahitaji fedha, utangamano na ushirikiano katika ngazi zote kwasababu changamoto za maji Duniani kama vile upungufu wa maji, ukame, mafuriko, uchafuzi na athari za mabadiliko ya tabianchi ni kubwa na zimeshavuka mipaka ya kiutawala.

*"Maji yanalazimisha jamii kuungana na kushirikiana."*

Amehitimisha kwa kualika nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jamuiya ya Kimataifa, Washirika wa Maendeleo, Wana Taaluma na Watafiti, Asasi za Karaia, na wadau wengine kushiriki katika kuhifadhi na kulinda Ziwa hilo.

*"Kila mmoja akiwa balozi mzuri wa uhifadhi wa ziwa Victoria kwa maana ya kufanya shughuli za uhifadhi na kuzuia shughuli hatarishi, tutafanikiwa."* ***Bi. Rose Ambrose***



Warsha imehudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka nje na ndani ya nchi ikiwa na kaulimbiu 'Maji Yetu, Mustakabali Wetu: Tuungane kwa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Victoria.





# Bonde La Ziwa Victoria ni Rasilimali Muhimu Afrika Mashariki.

*Mwanza*

Bonde la ziwa Victoria linaendelea kuwa moja ya maeneo muhimu zaidi kiuchumi na kiikolojia katika ukanda wa Afrika Mashariki kutokana na mchango wake katika sekta za uvuvi, usafirishaji, kilimo, biashara, utalii, uzalishaji wa nishati pamoja na huduma ya maji kwa mamilioni ya wananchi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Bi.Rose Ambrose amesema wakati wa majadiliano kuhusu maendeleo endelevu ya Bonde la ziwa Victoria, ambapo alieleza kuwa pamoja na umuhimu wa ziwa hilo, bado zipo changamoto mbalimbali ikiwemo uchafuzi wa mazingira, uvuvi haramu, magugu vamizi, ukataji miti, ongezeko la watu pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi.



Amesisitiza kuwa changamoto hizo zinahitaji ushirikiano wa pamoja kati ya nchi za ukanda huo pamoja na wadau mbalimbali ili kuhakikisha Ziwa Victoria linaendelea kuhifadhiwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Amesema Tanzania itaendelea kuimarisha ushirikiano na nchi jirani katika kuhakikisha maendeleo endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria yanafikiwa kupitia mshikamano, uwajibikaji wa pamoja na ushirikiano wa kikanda.




# Tuzo Zatolewa Siku Ya Ziwa Victoria

Kuelekea Siku ya Ziwa Victoria Kulikuwa na zoezi la utoaji wa tuzo kuwatambua waliochangia katika utunzaji na uendelezaji wa rasilimali maji katika ziwa Victoria.

Mgeni rasmi aliyekabidhi tuzo hizo ni Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb).

Tuzo zimelenga kutambua mchango, ubunifu na uwajibikaji katika kuhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika ziwa Victoria.







*Limeandaliwa na*

**Kitengo cha Mawasilianoa Serikalini, Wizara ya Maji**


Ps@maji.go.tz

+255 26 2322602

www.maji.go.tz

@wizarayamajitz


**LAKE VICTORIA DAY**
**2026**